

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

ALI MCHUMO SEKONDARI,
S.L.P 47,
KILWA MASOKO.
8/12/2020.

Kumb. Na. AMSS/S.1915/F.1/J.1/2019/14

MZAZI/MLEZI WA

.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI.

Mada ya hapo juu yahusika.

Nakujulisha kwamba kijana/ Binti yako mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari **Ali Mchumo**. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021.

SARE ZA DARASANI

A. WAVULANA

- Suruali mbili (2) nyekundu , Tafadhali suruali zisibane (modo) hazitakiwi kabisa.
- Mkanda mweusi usio na mapambo ya aina yoyote.
- Mashati meupe mawili mikono mifupi yasibane na yanayoweza kuchomekewa.
- Viatu vyeusi jozi mbili vyenye kamba (gidamu).
- Tai nyekundu mbili.
- Soksi nyeupe jozi mbili.

B. WASICHANA

- Sketi nyekundu mbili (2) sketi ziwe ndefu mpaka ziguse visigino.
- Blauzi (Nusu kanzu) mbili nyeupe za mikono mirefu.
- Hijabu nyeupe mbili zisizo na mapambo ya aina yoyote na zisizoonyesha (Transparent)
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Viatu vyeusi jozi mbili vyenye kamba (gidamu) za kufungia (Tafadhali haturuhusu uvaaji wa vibajaji au yebo yebo au kandambili labda kama anakidonda mguuni atatoa taarifa kwa walimu.

C. VIFAA VYA USAFI VYA KAZI ZA NJE ZA KUZALISHA MALI (ELIMU YA KUJITEGEMEA)

- (i) Wavulana waje na **fyekeo** ambazo zimeshanolewa.
- (ii) Wasichana waje na **ndoo ndogo** za plastiki (visado).

SARE ZA MICHEZO NA KAZI ZA NJE

Shule imeandaa utaratibu wa upatikanaji wa T-Shirt maalum zenye nembo ya shule zitauzwa kwa bei ya shilingi elfu kumi Tsh. (10,000/=).

VIFAA VYA DARASANI

- Daftari kubwa (Counter book) tisa (9).
- Kalamu ya wino (peni) za kutosha.
- Kalamu ya risasi (penseli).
- Mkebe uliotimia vifaa vyake (Mathematical set).
- Begi la kubebea na kutunzia vifaa vya darasani.
- Rim (bunda la karatasi nyeupe A₄ kwaajili ya mitihani ya wiki na ya mwezi).

NB:- Vifaa vyote vilivyoagizwa katika barua hii mwanafunzi na mzazi wajenavyo shuleni siku ambayo mwanafunzi ataletwa shuleni ili vikaguliwe.

AFYA YA MWANAFUNZI

Ndugu Mzazi au Mlezi kabla hujamleta kijana/Binti yako shule unatakiwa umpeleke kwanza Hospitali kwa ajili ya vipimo vya magonjwa mbali mbali, na Daktari atajaza fomu ilioambatanishwa baada ya kumpima mtoto.

SHERIA ZA SHULE

Sheria za Shule zimeambatanishwa katika barua hii. Mzazi na Mwanafunzi mnatakiwa kuzisoma kwa makini na kuzielewa.

Ahsante,

.....

ALLI MAHMOUD

MKUU WA SHULE